**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**MEI 2016**

## YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI……………………………………………………………………3

2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016………………………………………………..5

2.1 MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016………………………………………………..7

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016……………………………..6

3.1 UCHAMBUZI WA TAARIFA KUHUSU UKUSANYAJI MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016……………………………………………………11

3.1.1 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI………………..13

4.0 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017……………………………………………………………………13

4.1 MAKADIRIO YA MAPATO YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017……………………………………………….14

4.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI……………………………………………18

5.1 TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA-FUNGU 55…………18

5.2 OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI-FUNGU 16…………….19

5.3 TUME YA KUREKEBISHA SHERIA-FUNGU 59………………………………20

5.4 DIVISHENI YA MASHTAKA-FUNGU 35………………………………………20

5.5 TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA-FUNGU 12…………………………20

5.6 WIZARA YA KATIBA NA SHERIA-FUNGU 41…………………………….22

6.0 HITIMISHO………………………………………………………………………22

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimwa Spika,** napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa fursa ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu,

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016**,** naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Katiba na Sheria ina jukumu la kusimamia bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria ina mafungu 6 ya bajeti ambayo ni;

I. **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria
II. **Fungu 55** – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
III. **Fungu 59** - Tume ya Kurekebisha Sheria
IV. **Fungu 35** - Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka
V. **Fungu 16** - Mwanasheria Mkuu wa Serikali
VI. **Fungu 12** - Tume ya Utumishi wa Mahakama

**Mhehimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo makubwa matano yafuatayo:

I. Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

II. Utekelezaji wa mapendekezo na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

III. Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

IV. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

V. Maoni na Ushauri wa Kamati

## 2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Tarehe 30 Machi, 2016 na kupokea Taarifa kuhusu Mradi unaohusu Ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vile vile Kamati ilipata Taarifa kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyopo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:

### i) Wizara ya Katiba na Sheria (Fungu 41)

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara ya Katiba na Sheria ilitengewa Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tisa Hamsini na Tisa, Laki Saba Kumi na Tisa Elfu (2,959,719,000) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Mbili (2,000,000,000) ni fedha za ndani na Shilingi Milioni Mia Tisa Hamsini na Tisa, Laki Saba Kumi na Tisa Elfu (959,719,000) ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2016 Wizara ilipokea na kutumia Shilingi Milioni Thelathini na Tatu, Laki Sita na Thelathini Elfu (33,630,000) ambbayo ni fedha za nje kupia Mradi wa **UNICEF Multi-sectoral Support.** Ofisi haikupokea fedha yoyote ya ndani kama ilivyoidhinishwa na Bunge ambazo zingesaidia katika utekelezaji wa mradi huu kikamilifu.

### ii) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ( Fungu 16)

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa Shilingi Milioni Mia Sita Arobaini na Nne, Laki Saba na Arobaini Elfu (644,740,000) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi Milioni Mia Tatu Arobaini na Nne, Laki Saba na Arobaini Elfu (344,740,000) ni Fedha za Ndani na Shilingi Milioni Mia Tatu (300,000,000) ni Fedha za Nje kutoka UNDP

**Mheshimiwa Spika**, fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Maendeleo zilikuwa ni kwa ajili ya kujengea uwezo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kusimamia masuala ya Mikataba mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mikataba ya Sekta ya Nishati na Madini kupitia ***Mradi wa Capacity Development in The Energy Sector and Extractive Industries*** (CADESE)

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu haukuweza kutekelezwa ipasavyo kwa sababu ya kukosekana kwa Fedha za nje kutoka **United Nations Development Programme** ambayo iliahidi kutoa Shilingi Milioni Mia Tatu (300,000,000) na hazikutolewa. Fedha liyotolewa ni Shilingi Milioni Mia Tatu Arobaini na Nne Elfu, Laki Saba Arobaini Elfu (344,740,000) tu kwa Mradi huu ambazo ni Fedha za ndani. Vile vile Ofisi hii imeshindwa kutekeleza Mradi wa ujenzi na Ukarabati wa Majengo yake kwa sababu ya kukosekana fedha.

### iii) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ( Fungu 55)

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa fedha 2015/2016 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilitengewa Shilingi Milioni Mia Mbili Arobaini na Sita, Laki Moja na Ishirini na Mbili Elfu (246,122,000) kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa **National Human Rights Action Plan** (NHRAP). Mradi huu unahusu Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Haki za Binadamu Nchini.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2016 kiasi kilichopokelewa kwa ajili ya Mradi huu ni Shilingi Milioni Mia Moja Themanini na Nane, Laki Mbili na Elfu Kumi na Mbili (188,212,000) sawa na asilimia 76 ya fedha yote iliyoidhinishwa. Hivyo Mradi huu haukutekelezeka kikamilifu kutokana na kutotolewa fedha zote zinazokidhi mahitaji ya utekelezaji wa mradi.

## 2.1 MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haijaridhishwa na kasi ya utoaji wa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwani karibu miradi yote imepokea sehemu tu ya fedha iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2015/2016. Kamati vilevile inasikitishwa na hatua ya Serikali kutotoa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Miradi mingi ya maendeleo imekua inategemea kwa kiasi kikubwa fedha za nje. Mfano, katika Fungu 16 Ofisi ilipokea fedha za nje tu kupitia UNICEF Multi-Sectoral Support program na haikupokea fedha yoyote kutoka ndani.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya kufanya Maendeleo, kuna umuhimu wa kila Taasisi ya Serikali kubuni vyanzo vya mapato vitakavyosadia kuongeza fedha za ndani ili kuepuka utegemezi wa fedha za nje.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ilikutana Jijini Dar es Salaam Tarehe 8 na 9 Aprili, 2016 kwa ajili ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara hii, Kamati ilizingatia mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Mwezi Mei 2015 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 ili kujua vipaumbele vya kibajeti katika Mwaka wa Fedha Ujao.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara ya Katiba na Sheria kwa ujumla ilidhiinishiwa Shilingi Bilioni Mia Moja Tisini na Moja, Milioni Mia Nne Hamsini, Laki Tisa na Moja (191,450,900,001) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia Mwezi Machi 2016, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Bilioni Tisini na Saba, Milioni Mia Mbili Hamsini na Tano, Laki Tano na Sita Elfu, Mia Mbili Thelathini na Tisa (97,255,506,239) sawa na asilimia 49 ya fedha zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**,fedha inayoombwa na Wizara ya Sheria na Katiba kwa Mafungu yote katika mwaka huu wa fedha ni Shilingi Bilioni Thelathini na Tano,Milioni Mia Saba Themanini na Tano,Mia Nne Kumi na Sita Elfu(35,785,416,000/=).Fedha hii ni mara tano pungufu ya fedha iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, Upungufu huu unatokana na kiasi kikubwa cha fedha iliyokua inatengwa chini ya Fungu 41 kuhamishiwa katika Fungu 40 (Mahakama) kutokana na Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015. Pia Upungufu huu unatokana na kupungua kwa fedha ya matumizi mengineyo kwa wizara na sekta zote ambao ni mwenendo wa bajeti katika mwaka huu wa fedha.

**Jedwali 01: Mlinganisho wa Fedha Iliyotengwa na Kupokelewa Katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Chini ya Fungu 41**

| **Fungu** | **Fedha Iliyoidhinishwa Sh.** | **Fedha Iliyopatikana Sh.** | **Tofauti Sh.** | **Asilimia Sh.** |
|---|---|---|---|---|
| 41 | Sh.191,450,900, 001 | Sh.97,255,506,239 | Sh.94,195,393,762 | 49 |

**Mheshimwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara mpaka sasa imepokea Asilimia 49 ya fedha iliyoidhinishwa. Kukosekana kwa kiasi hicho kikubwa cha fedha katika Wizara hii kutakuwa kumeathiri utekelezaji wa majukumu muhimu na ya msingi. Kamati inaona kuwa kuna umuhimu wa kuisisitiza Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa kwa wakati ili majukumu ya Wizara hii yaweze kutekelezeka kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 hadi kufikia Machi 2016 katika mafungu sita

yanayosimamiwa na Wizara yaani Fungu 41, 16, 35, 59,55 na 12 umeainishwa kwenye majedwali hapa chini kwa kila Fungu

1) **Wizara ya Katiba na Sheria (Fungu 41)(Jedwali 02)**

| | **Fedha Zilizoidhinishwa** | **Fedha Zilizopokelewa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Kawaida | Sh. 4,182,321,000 | Sh. 1,159,151,385 | 28 |
| Mishahara | Sh. 5,268,767,000 | Sh. 3,051,795,520 | 58 |
| Maendeleo | Sh. 2,959,719,000 | Sh. 118,276,750 | 3.9 |
| Jumla | Sh.12,410,807,000 | Sh.4,329,223,655 | 35 |

2) **Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Fungu 16)(Jedwali 03)**

| | **Fedha Zilizoidhinishwa** | **Fedha Zilizopokelewa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| **Kawaida** | Sh.4,784,217,000 | Sh.2,045,921,885 | Sh.43 |
| **Mishahara** | Sh.3,759,244,500 | Sh.2,506,163,000 | Sh.66 |
| **Maendeleo** | Sh.300,000,000 | Sh.344,740,000 | Sh.115 |
| **Jumla** | Sh.8,843,461,500 | Sh.4,896,824,885 | Sh. 55 |

**3) Divisheni ya Mashitaka (Fungu 35)(Jedwali 04)**

| | **Fedha Zilizoidhinishwa** | **Fedha Zilizopokelewa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| **Kawaida** | Sh. 7,160,742,000 | Sh. 2,584,486,151 | 36 |
| **Mishahara** | Sh.922,251,800 | Sh.6,148,345,545 | 666.7 |
| **Maendeleo** | Sh. 342,884,000 | Sh. 342,884,000 | 100 |
| **Jumla** | 8,425,877,800 | Sh. 9,075,715,696 | 107 |

**4) Tume ya Utumishi wa Mahakama (Fungu 12) (Jedwali 05)**

| | **Fedha Zilizoidhinishwa** | **Fedha Zilizopokelewa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| **Kawaida** | Sh. 2,017,276,000 | Sh. 322,050,463 | 16 |
| **Mishahara** | Sh. 668,916,000 | Sh. 67,134,000 | 10 |
| **Maendeleo** | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | Sh. 2,686,192,000 | Sh. 389,184,463 | 14.58 |

### 4) Tume ya Kurekebisha Sheria (Fungu 59) (Jedwali 06)

| | **Fedha Zilizoidhinishwa** | **Fedha Zilizopokelewa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| **Kawaida** | Sh. 1,755,874,961 | Sh. 430,474,863 | 25 |
| **Mishahara** | Sh. 1,229,817,000 | Sh. 2,985,691,961 | 242 |
| **Maendeleo** | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | Sh. 2,985,691,961 | Sh. 828,362,938 | 28 |

### 6) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) (Jedwali 07)

| | **Fedha Zilizoidhinishwa** | **Fedha Zilizopokelewa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| **Kawaida** | Sh. 2,226,368,000 | Sh. 740,962,701 | 33 |
| **Mishahara** | Sh. 2,779,581,000 | Sh. 1,536,418,700 | 55 |
| **Maendeleo** | Sh. 572,389,000 | Sh. 294,506,000 | 51 |
| **Jumla** | Sh. 5,578,338,000 | Sh. 2,571,887,401 | 46.1 |

**MheshimiwaSpika**,mwenendo huu wa upokeaji fedha kwa ujumla unaonyesha kwamba fedha inayopokelewa ni ndogo sana ukilinganisha na kiasi kinachoidhinishwa na Bunge lako tukufu. Hii inaonyesha kwamba Taasisi nyingi zinashindwa kumudu majukumu yao kwa wakati na ufanisi kutokana na fedha kuchelewa kutoka Hazina**.**

## 3.1 UCHAMBUZI WA TAARIFA KUHUSU UKUSANYAJI MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara ya Katiba na Sheria kwa pamoja na Taasisi zake ilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Ishirini na Tatu, Laki Tisa Thelathini na Tatu,Mia Saba Hamsini (17,023,933,750) kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia Februari, 2016 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Moja Kumi na Sita, Laki Nane Arobaini na Tisa Elfu, Mia Nane Kumi na Moja (11,116,849,811) ikiwa ni sawa na asilimia 65 ya makusanyo yaliyotarajiwa kama ilivyochanganuliwa hapa chini:

**Jedwali 08: Mlinganisho wa Makadirio, Makusanyo na Asilimia Kwa Mafungu Yaliyo Chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016**

| Fungu | Makadirio | Makusanyo | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 12 | Sh. 0 | 0 | 0 |
| 16 | Sh. 1,002,000 | Sh. 3,255,000 | 325 |
| 35 | Sh. 13,002,000 | Sh. 12,000,000 | 92 |
| 40 | Sh. 5,203,298,719 | Sh. 5,789,939,272 | 111 |
| 41 | Sh. 11,801,400,000 | Sh. 5,890,822,355 | 50 |
| 55 | Sh. 5,131,000 | 0 | 0 |
| 59 | Sh. 100,000 | 0 | 0 |
| Jumla | Sh. 17,023,933,719 | Sh. 11,696,016,627 | 65 |

**Mheshimiwa Spika**, makusanyo haya ni kutokana na ada za Usajili wa Matukio, Ada za wanafunzi, uuzaji wa vitabu vya zabuni na huduma nyingine mbalimbali zinzotolewa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Katiba na Sheria, Fungu 41 imeongoza katika ukusanyiji wa Maduhuli kwa kukusanya Shillingi Bilioni Tano, Milioni Mia Nane Tisini, Laki Nane Ishirini na Mbili Elfu (5,890,822,355) ikifuatiwa na Idara ya Mahakama iliyokusanya Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Mbili na Kumi, Laki Saba Sabini na Saba na Mbili, Mia Nne Hamsini na Saba (5,210,772,457). Iliyofuatia katika kukusanya maduhuli ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali Fungu 16 iliyokusanya Shilingi Milioni Tatu, Laki Mbili Ishirini na Tano Elfu (3,255,000).

**Mheshimiwa Spika**, Mafungu mengine yalikuwa na matarajio ya kukusanya maduhuli lakini matarajio hayakuwa kama yalivyopangwa. Hii ni changamoto ambayo Wizara na Taasisi zote zenye vyanzo vya mapato zinabidi kuiangalia kwa umakini kwani matarajio sio mapato.

**Mheshimiwa Spika**, makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha uliopita haukuendana na matarajio ya Wizara. Matarajio ya Wizara yalikuwa makubwa lakini kilichopatikana ni kidogo. Hivyo kuna umuhimu wa kuweka vyanzo vingine vya ukusanyaji wa maduhuli ili kuongeza upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hasa kwa zile Taasisi zilizokosa mapato kabisa.

### 3.1.1 **MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uwasilishaji wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo ishirini na saba (27) kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa mapendekezo yote yametekelezwa isipokuwa moja ambalo linahusu deni la RITA. Katika Mwaka 2015/2016 Kamati iliishauri Serikali kulipa fedha inazodaiwa na RITA ili RITA iweze kutekeleza majukumu yake katika Mkataba wa Ubia wa jengo la RITA TOWER ili kuepukana na ongezeko la riba. Kamati imeelezwa kuwa kutokana na changamoto za kibajeti Serikali imeshindwa kulipa deni hilo na inafanya jitihada ili fedha hizo zipatikane.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inazidi kuisisitizia Serikali kulipa deni hilo mapema ili kupunguza ongezeko la riba kutokana na kutolipwa kwa deni hili.

## 4.0 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Katiba na Sheria imejiwekea malengo kumi na moja (11) ya utekelezaji ili kuongeza ufanisi na ubora katika kutoa huduma za kisheria na masuala ya Katiba. Malengo hayo ni:-

i) Kuimarisha usimamizi na uratibu wa mfumo wa Sheria;

ii) Kuratibu uanzishwaji na uendeshaji wa Divisheni ya Mahakama ya Rushwa na Ufisadi ili kuharakisha usikilizaji wa Mashauri;

iii) Kuratibu uundaji na uendeshaji wa Kamati ya kusimamia utekelezaji wa masharti yatokanayo na masharti ya mpito kwenye katiba inayopendekezwa;

iv) Kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundobinu ya huduma za mahakama na Taasisi zake;

v) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kutoa huduma mbalimbali na kutunza kumbukumbu muhimu;

vi) Kuimarisha shughuli za utafiti wa sheria na kufanya marekebisho ya sheria zilizopitwa na wakati;

vii) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi na kuendeleza watumishi kitaaluma;

viii) Kuimarisha huduma za Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo ikiwa ni pamoja na kuongeza udahili wa wanafunzi na kupanua wigo wa huduma kwa walengwa;

ix) Kuweka wigo mpana wa sheria na upatikanaji wa msaada wa kisheria (Legal Aid Services) kwa watu wasio na uwezo;

x) Kuimarisha mifumo ya utunzaji nyaraka , kumbukumbu na takwimu; na

xi) Kuimarisha shughuli za usajili na utunzaji wa kumbukumbu (Civil Registration and Vital Statistics)

**Mheshimiwa Spika**, malengo ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii yameongezeka ukilinganisha na malengo waliyojiwekea katika Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na malengo ya Wizara kwa ujumla kwani yanalenga katika kuboresha utekelezaji wa majukumu na kuleta ufanisi zaidi katika suala zima la utoaji haki nchini.

### 4.1 MAKADIRIO YA MAPATO YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nane, Tisini na Sita, na Ishirini Elfu, (**11,896,020,000/=**) ikiwa na Maduhuli ya Serikali, kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:

| **Fungu** | **Matarajio ya Maduhuli (Sh.)** |
|---|---|
| 12 | 0 |
| 16 | 1,002,000 |
| 35 | 13,002,000 |
| 41 | 11,882,012,000 |
| 55 | 0 |
| 59 | 4,000 |
| **Jumla** | **11,896,020,000/=** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Makadirio ya Mapato hayaendani na hali halisi ya makusanyo. Hivyo Kamati inashauri kuwa ni vizuri Serikali ikaweka makadirio madogo yenye uhakika kuliko kuweka matarajio makubwa ambayo mwisho wa siku hayakusanywi.

**Mheshimiwa Spika,** Fungu 55 (Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora) na Fungu 12 (Tume ya Utumishi wa Mahakama) hayana matarajio yoyote ya kukusanya maduhuli kwa sababu ya kutokuwa na vyanzo vya mapato.

## 4.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara imeomba kuidhinishiwa kiasi cha Shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Saba Themanini na Tano, Mia Nne Kumi na Sita Elfu (35,785,416,000) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| i) | Mishahara ya Watumishi | Sh. | 22,391,694,000 |
| ii) | Matumizi Mengineyo | Sh. | 10,619,234,000 |
| iii) | Miradi ya Maendeleo | Sh. | 2,774,488,000 |
| | **Jumla** | **Sh.** | **35,785,416,000** |

**Mheshimiwa Spika,** fedha zinazoombwa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ni sawa na asilimia 0.1 ya Bajeti Kuu ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ambayo ni Trilioni 29.

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria katika mafungu sita (6) unaonyesha jumla ya fedha zitakazotumika katika Mwaka wa Fedha ujao ikijumuisha Matumizi ya Mishahara, Matumizi Mengineyo pamoja na Matumizi ya Fedha za Maendeleo za Nje na Ndani kwa ujumla katika kila Fungu kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini.

**JEDWALI 09: MCHANGANUO WA MATUMIZI KWA KILA FUNGU**

| Fungu | Jumla Ya Matumizi |
|---|---|
| 12 | Sh. 1,134,955,000 |
| 16 | Sh. 6,997,324,000 |
| 35 | Sh. 13,299,639,000 |
| 41 | Sh. 9,137,717,000 |
| 55 | Sh. 3,557,589,000 |
| 59 | Sh. 1,658,192,000 |
| **Jumla** | **Sh. 35,785,416,000** |

**Mheshimiwa Spika**, Divisheni ya Mashitaka (Fungu 35) lina makadirio ya matumizi ya juu zaidi ikilinganishwa na mafungu mengine. Bajeti inayoombwa kwa ajili ya Fungu hili ni sawa na asilimia 37% ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Utumishi wa Mahakama (Fungu 12) lina Makadirio ya Matumizi madogo zaidi ikilinganishwa na mafungu mengine ikiwa ni sawa na asilimia 3.2% ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) inaombewa Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tano Hamsini na Tano, Mia Tano Themanini na Tisa Elfu (3,557,589,000). Wakati Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inawasilisha Taarifa kwenye Kamati Tarehe 8 Aprili, 2016 ilibainika kuwa fedha zilizotengwa zinakidhi Mishahara, Malipo ya Pango la Ofisi na malipo mengine madogo madogo. Hivyo kwa Bajeti inayoombwa haiwezeshi Tume kutekeleza majukumu yake ya Msingi yaliyowekwa Kikatiba, kama vile kuhamasisha haki za Binadamu nchini, kufanya uchunguzi juu ya uvunjwaji wa Haki za Binadamu na kadhalika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekutana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora mara tatu kati ya Februari na Aprili 2016 na kujadili kwa kina uwezo wa kifedha wa Tume katika kutimiza majukumu yake ya kikatiba. Baada ya kuwa imejiridhisha vya kutosha kwamba fedha iliyotengwa kwa ajili ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika mwaka huu wa fedha kuwa ni ndogo sana ukilinganisha mahitaji halisi ya Tume, Kamati iliamua kupeleka Ombi maalumu katika Kamati ya Bajeti ya Bunge ili bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Tume ya Haki za Binadamu katika mwaka huu wa fedha iongezwe kwa Sh. Bilioni Mbili zaidi kutoka Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tano Hamsini na Saba, Mia Tano Themanini na Tisa Elfu.(3,557,589,000).

**Mheshimiwa Spika,** katika kusisistiza umuhimu wa Tume hii kuongezewa fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kikatiba, tarehe 4 Mei, 2016 Mwenyekiti wa Kamati hii ya Katiba na Sheria aliwasilisha maombi mbele ya Kamati ya Bajeti ya nyongeza ya Shilingi Bilioni Mbili (2,000,000,000,000) katika Bajeti ya Mwaka 2016/2017. Suala hili lilijadiliwa kwa kirefu kwenye Kamati ya Bajeti na Waziri wa Katiba na Sheria, watendaji wa Wizara ya Katiba na Sheria na Kamishna wa Fedha walihudhuria. Baada ya majadiliano ya kina Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti aliahidi kulijadili kwa undani suala hili na kuahidi kutoa maamuzi baadae.

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala katika mwaka 2016/2017 inaombewa kiasi cha Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tano Hamsini na Tano, Mia Tano Themanini na Tisa Elfu( **3,557,589,000).** Kati ya fedha hizo shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tatu Themanini na Tatu, Mia Moja Kumi na Sita Elfu (**2,383,116,000)** ni kwa ajili ya mishahara (PE) na shilingi **994,514,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Kati ya fedha hizi za matumizi mengineyo shilingi Milioni Miatatu Ishirini (**320,000,000.00)** zimetengwa na kuzuiwa kwa ajili ya kulipa pango, hivyo Tume inabakiwa na Shilingi Milioni Mia Sita Sabani na Nne, Mia Tano Kumi na Nne Elfu (674,514,000) za utekelezaji wa majukumu yake. Kiasi hiki hakitaweza kukidhi hata mahitaji ya uendeshaji wa ofisi. Ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa hapo chini, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Kamati inashauri Serikali kuiongezea Tume kiasi cha Shilingi Bilioni Mbili (**2,000,000,000.00)** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Kwa bajeti hii ndogo iliyoombwa Watumishi wa Tume watapokea mishahara tu bila kufanya kazi yoyote kwa mwaka mzima.

**Mheshimiwa Spika**, maeneo ya kipaumbele kwa Tume yenye kugusa moja kwa moja haki za binadamu ambayo hayakutengewa fedha yoyote ni kama ifuatavyo;

i) Kufuatilia haki za makundi maalum katika jamii kama watoto, watu wenye ulemavu, wazee na kutoa elimu kwa Umma;

ii) Kufuatilia na Kushughulikia Malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu;

iii) Kuimarisha Mahusiano na Wadau wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;
iv) Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi;
v) Nyongeza ya gharama za utendaji na kuendesha ofisi;

**Mheshimiwa Spika**, maeneo ambayo hayajatengewa fedha hapo juu ni kati ya majukumu ya msingi ya Tume ambayo yalipaswa kupewa kipaumbele. Hivyo, kwa msingi huu, Kamati inaona kuwa fedha inayoombwa kwa ajili ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni ndogo na haitaweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati pamoja na majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao ili kuboresha utendaji kazi kwa lengo la kuleta ufanisi kwa manufaa ya Taifa.

### 5.1 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55)

- Serikali itoe fedha za kutosha kwa Tume ili iweze kutimiza majukumu yake ya Kikatiba kwa ufanisi

- Serikali iongeze Ofisi za Tume katika Mikoa mingi zaidi Tanzania Bara na Zanzibar na hasa Pemba ambapo Tume bado haijaweza kuanza kufanya kazi kutokana na ufinyu wa bajeti.Kwa upande wa Tanzania Bara Tume iongeze ofisi zaidi katika Kanda ya Ziwa ambapo kumekua na matukio mengi ya ukiukwaji wa haki za Binadamu hasa maeneo ya migodini.

- Serikali ihakikishe kwamba fedha iliyotengwa kwa ajili ya Tume inatolewa kwa wakati.

- Kamati inaishauri Serikali kufuata sheria zilizowekwa katika kutekeleza majukumu yake kwa sababu kuna sheria ambazo inaonekana utekelezaji wake ni mgumu kwa mfano adhabu ya kifo Hivyo Kamati inashauri kama kuna sheria ambazo utekelezaji wake ni mgumu zifanyiwe marekebisho. Hii itaendana na Itifaki ya Pili ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa Mwaka 1966 unaozitaka nchi wanachama wa Mkataba huu kuondoa adhabu ya

kifo. Ingawa Tanzania bado haijaridhia Itifaki hii ya Mwaka 1989, Kamati inaishauri Serikali kuridhia Itifaki hii na kutunga sheria ambayo itaondoa adhabu ya Kifo. Hatua hii ni muhimu kwa sababu Tanzania tayari imeridhia Mkataba huu wa mwaka 1966 na Kamati inashauri Serikali kuridhia Itifaki hii ya mwaka 1989 iliyo chini ya Mkataba huu wa mwaka 1966.

## 5.2 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Fungu 16)

- Serikali ianzishe mapema iwezekanavyo mchakato wa kujenga Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria na Wawekezaji wengine kama NSSF
- Serikali itenge bajeti ya kutosha itakayowezesha kuwajengea uwezo na ujuzi watumishi wa ofisi hii na kuwapatia mafunzo ya kisasa katika Nyanja mbalimbali ili waendane na mabadiliko ya teknolojia kulingana na Taaluma zao.
- Kwa kuwa sasa nchi inaingia katika uchumi wa gesi Kamati inaishauri Serikali kujenga uwezo wa Wanasheria wa Serikali ili wabobee katika Sheria za Mafuta na Gesi na hasa eneo la mikataba ya sekta hii.Hii itaongeza uwezo wa serikali katika kujadili na kusimamia maslahi ya taifa na kupunguza uwezekano wa kuhujumiwa na makampuni makubwa yaliyowekeza katika sekta ya gesi na mafuta.

## 5.3 Tume ya Kurekebisha Sheria (Fungu 59)

- kutokana na ufinyu wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti kwa Tume ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.
- Serikali Iendelee kuthamini kazi kubwa inayofanywa na Tume kwa kuyafanyia kazi mapendekezo yanayotolewa ili kuboresha sheria za nchi. Aidha, Tume iendelee kufanya Tafiti kuhusu sheria mbalimbali ambazo kutokana na mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi

zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili ziweze kuendana na wakati wa sasa.

- Kamati inashauri Serikali kufanyia kazi kwa haraka taarifa za utafiti za Tume hasa kuhusu Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ambayo inakinzana na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 kuhusu umri wa mtoto ili kulinda haki zote za mtoto (***Best Interests of the Child***) na hasa haki ya kila mtoto kupata elimu,kuwa na afya njema na kutokuolewa mapema. Lakini pia, kamati inaishauri serikali kupitia na kufanyia kazi taarifa na sheria zote zilizowasilishwa na Tume zinazohitaji maboresho ili kuendana na wakati.

## 5.4 Divisheni ya Mashitaka (Fungu 35)

- Serikali kuendelea kuajiri Mawakili wa Serikali wa kutosha ili kukabiliana na wingi wa kesi kutokana na ongezeko la uhalifu. Aidha, maslahi ya watumishi hao yaboreshwe ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Vilevile, kamati inasisitiza juu ya ujenzi wa nyumba za Mawakili wa Serikali ili waweze kuishi kwenye makazi salama ukizingatia kuwa wanashughulikia kesi za mbalimbali ambazo zinahusisha matukio makubwa ya uhalifu kama mauaji na kadhalika

## 5.5 Tume ya Utumishi wa Mahakama (Fungu 12)

- Serikali ione umuhimu wa kuiongezea Tume hii fedha kwa kulingana na majukumu yake**.**
- Kutokana na kutokukamilika kwa matengenezo ya vyumba vya ofisi katika jengo la RITA ambao unasababisha Mwenyekiti wa Tume, Wajumbe na Makamishna kukosa Ofisi mahsusi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao, Kamati inaishuri Serikali kutenga fedha za kutosha ili Ofisi zilizopo kwenye Jengo la RITA zikamilike kwa haraka.
- Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili Tume hii iweze kushughulikia kikamilifau malalamiko ya ukiukwaji wa maadili na nidhamu kwa Watumishi wa Mahakama.

- Kamati inaishauri Serikali kufuata Sheria za NACTE za uanzishwaji wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), ambazo zinataka Mkuu wa Chuo na Msaidizi wake kuwa na Shahada ya Uzamivu. (Ph. D )

- Kamati inaishauri Serikali kukiboresha Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto ili kiweze kutoa wahitimu mahiri katika fani ya Sheria katika kiwango cha Cheti, Stashahada na Shahada.Ili kufikia lengo hili Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba mkuu wa chuo na wahadhiri wengine wana viwango vya elimu vinavyokubalika katika kufundisha vyuo vikuu Tanzania hasa kiwango cha Uzamivu na Uzamili.

- Ili kusimamia Haki katika ubora unaotakiwa Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba idadi ya kesi walizopangiwa mahakimu na majaji kwa mwaka hakuathiri ubora wa hukumu wanazotoa na usimamizi wa haki mahakamani.Kamati inatambua kwamba Dhana ya ***‘’Justice Delayed is Justice Denied’’*** ni muhimu katika utoaji haki lakini ni muhimu pia kwa watendaji wa Mahakama kuzingatia dhana ya ***‘’Justice Hurried is Justice Buried’’*** katika kusimamia Haki.Hivyo kamati inashauri mahakimu,majaji na watendaji wa mahakama kuhakikisha kwamba haki inasimamiwa katika ubora wake na siyo katika wingi wa kesi zinazoamuliwa na mahakama.

- Kamati inaishauri Serikali Kuboresha Miundo Mbinu ya Mahakama Hasa mahakama za Mwanzo na Wilaya ili kuboresha mazingira na ufanisi wa utoaji Haki nchini.

- Kamati inaishauri serikali kulipia gharama za nyumba na posho ya kutokufanya shughuli binafsi za Sheria (Rent Assistance and Non-practicising Allowance) kwa Mahakimu 1224 walioajiriwa na Mahakama kama ilivyo kwa wanasheria wa Serikali.

- Kamati inaishauri Tume ya Utumishi wa Mahakama kuendelea kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa watumishi wa Mahakama wasiozingatia Maadili ya Kazi na kuhakikisha kwamba watumishi hao wanawajibishwa kwa mujibu wa Sheria.

## 5.6 Wizara ya Katiba na Sheria (Fungu 41)

- Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kuhuisha mchakato wa kupata Katiba mpya kutokana na mapendekezo yaliyotolewa katika mchakato wa kupata katiba uliosimama mwaka 2014 Oktoba. Kamati inasisitiza kwamba ni muhimu kwa Serikali kutenga fedha au kuongeza fedha ya nyongeza katika mwaka huu wa fedha ili kumalizia mchakato wa Tanzania Kupata Katiba mpya.

- Kwa kuzingatia majukumu muhimu ya Wizara hii, Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha Wizara kwa kuitengea bajeti ya kutosha na kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatolewa kwa wakati.

- Kwa kuwa Taasisi nyingi za Wizara hii Ofisi zake ziko katika majengo ya kupanga hali inayosababisha Wizara kutumia fedha nyingi kwa ajili hiyo, Kamati inashauri Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga majengo yake ili kuepuka gharama za upangaji.

- Kamati inaishauri Wizara ya Katiba na Sheria kujikita katika mifumo ya kielectroniki ili kuboresha ufanisi katika sekta ya Sheria na miundo mbinu ya utoaji haki.

- Kamati inaishauri Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake kuwa wabunifu katika kubuni miradi mbalimbali katika sekta ya Sheria itakayoongeza ufanisi katika sekta hii na ambayo itaongeza maduhuli ya wizara kuliko kuendelea kutegemea wahisani katika bajeti zao za maendeleo

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Aidha, hatuna budi kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara, umakini na umahiri mkubwa. Napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria

Dr.Harrison Mwakyembe, Mb, Katibu Mkuu Prof.Sifuni Ernest Mchome,Naibu Katibu Mkuu Ndugu Amon Mpanju na Watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio na Matumizi Wizara ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Uzalendo na uchapakazi wao pamoja na ushirikiano mkubwa walionipa umesaidia kufanikisha kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati. Kwa ruhusa yako naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:

(i) Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb, Mwenyekiti

(ii) Mhe. Najma Mutraza Giga, Mb, Makamu Mwenyekiti

(iii) Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb, Mjumbe

(iv) Mhe. Ally Saleh Ally, Mb, Mjumbe

(v) Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb, Mjumbe

(vi) Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb, Mjumbe

(vii) Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb, Mjumbe

(viii) Mhe. Seif Ungando Ally, Mb, Mjumbe

(ix) Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb, Mjumbe

(x) Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb, Mjumbe

(xi) Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb, Mjumbe

(xii) Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb, Mjumbe

(xiii) Mhe. Dkt. Godwin Aloyce Mollel, Mb, Mjumbe

(xiv) Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb, Mjumbe

(xv) Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb, Mjumbe

(xvi) Mhe. Omary Ahmed Badwel, Mb, Mjumbe

(xvii) Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb, Mjumbe

(xviii) Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb, Mjumbe

(xix) Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb, Mjumbe

(xx) Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb, Mjumbe

(xxi) Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb, Mjumbe

(xxii) Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb, Mjumbe

(xxiii) Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb, Mjumbe

(xxiv) Mhe. Dkt Mathayo David Mathayo, Mb, Mjumbe

Aidha napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt Thomas D. Kashillah, Katibu wa Bunge, kwa kusaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza Majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndugu Angelina Sanga, Stella Bwimbo, Dunford Mpelumbe na Gaitana Chima kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Sheria na Katiba.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Hoja.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

**05 Mei, 2016**